

# SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA



## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI UUZWAJI WA NYUMBA ZA KIGAMBONI HOUSING ESTATE, KIGAMBONI, DAR ES SALAAM

Kwa mara nyingine tena Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) leo tarehe 20 Desemba, 2012 linawatangazia mchakato wa kuanza rasmi kupokea maombi ya kununua nyumba ifikapo tarehe 2 Januari 2013, katika mradi wake mpya wa Kigamboni Housing Estate zilizopo Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Ujenzi wa nyumba hizi ulianza Novemba Mosi 2012 ukihusisha awamu mbili za ujenzi zenye jumla ya nyumba 290 na utakamilika mapema mwezi Mei 2013.

Mradi unatarajiwa kugharimu kiasi cha zaidi ya Shilingi bilioni 6.6 mpaka utakapomalizika, fedha zinazogharamiwa na Shirika kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo fedha za mikopo kutoka taasisi za fedha.

Jiwe la msingi la mradi huu liliwekwa rasmi tarehe 13 Desemba, 2012 na Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania. Uwekaji wa jiwe la msingi, unaashiria pia kuanza kwa miradi mingine ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu inayotekelezwa na Shirika katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri za Wilaya hivi sasa.

Sifa za msingi za mradi huu zinajumuisha huduma muhimu za jamii kama sehemu ya shule, maduka, zahanati, sehemu za kuchezea watoto na sehemu za wazi Katika awamu hii ya kwanza jumla ya nyumba 182 zitauzwa kwa wananchi wa kipato cha chini ili kuwawezesha kutimiza ndoto yao ya kumiliki nyumba. Wananchi hao wataweza kukopa fedha za kununulia nyumba hizi kutoka kwenye benki zilizoingia makubaliano na Shirika la Nyumba la Taifa.

Pia Mradi unatarajiwa kuboresha maisha ya wanunuzi wa nyumba hizi kwani upo karibu kabisa na jiji na kwamba mnunuzi anaweza kwenda kazini bila kutumia gharama kubwa ya usafiri wa gari.

Nyumba hizo 182 zitakazouzwa ni za aina mbili ambazo ni nyumba ya vyumba vitatu na ya vyumba viwili. Nyumba ya vyumba vitatu ina ukubwa wa mita za mraba 70 huku nyumba ya vyumba viwili ikiwa na ukubwa wa mita za mraba 56.

Sifa za ziada za mradi huu ni kuwa na chumba kimoja kinachojitegemea kwenye nyumba ya vyumba vitatu, kila nyumba ina sebule na sehemu ya kulia chakula, ramani ya ukuta unaotenganisha mipaka kati ya maeneo ya wakazi (wakazi wanaweza kujenga ukuta unaowatenganisha kulingana na michoro), na jiko la nje.

Kila nyumba ya vyumba viwili inauzwa kwa **TZS 39,816,565.62 bila kodi ya ongezeko la thamani** wakati nyumba ya vyumba vitatu itauzwa kwa bei ya **TZS 45,567,517.34 bila kodi ya ongezeko la thamani**.

Kupitia mkutano huu, tunawahamasisha na kuwakaribisha watanzania wote walio nchini na nje ya nchi kujiandaa ili ifikapo tarehe 2 Januari, 2013 wajitokeze kuomba na kuanza kulipia ununuzi wa nyumba hizo. Tumeweka muda huo wa wiki mbili hivi ili kuwaandaa wananchi wanaotaka kununua nyumba hizo.

Ifikapo wakati huo wanunuzi watarajiwa wanaweza kufanya mawasiliano na Makao Makuu ya Shirika, Ofisi zetu za Mikoa au kupitia baruapepe na kukamilisha taratibu mapema kwa ajili ya kuweza kuingia kwenye mchakato ulio wazi wa manunuzi.

Katika kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba, Shirika linajenga nyumba za gharama ya juu, kati na chini ili kuwahudumia wataanzania wa kada zote. Katika azma hiyo, nyumba 10,000 zitakazojengwa kufikia 2015 zitahusu watu wa kipato cha juu na nyumba 5,000 zitakazojengwa kufikia mwaka huo zitakuwa ni nyumba za watu wa kipato cha chini.

Shirika katika awamu ya kwanza limeanza kujenga nyumba za gharama nafuu katika maeneo mengine nchini ambayo maandalizi ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu yameanza ni Mvomero (Morogoro), Ilembu (Katavi), Geita, Mkinga (Tanga), Babati (Manyara), Monduli na Longido (Arusha), Unyankuni (Singida), Mtanda (Lindi), Kongwa (Dodoma), Iwambi (Mbeya), Mlote (Kigoma) na Mkuzo (Songea). Karibu Mikoa yote itakuwepo katika utekelezaji wa Mpango wa kujenga nyumba za gharama nafuu.

Ukiwa mdau na mnunuzi mtarajiwa, ama una ndugu/rafiki anayetamani kununua nyumba katika mradi huu, tumia kipindi hiki cha wiki mbili kujiandaa ili ifikapo tarehe 2 Januari 2013 uweze kutuma maombi na kulipa pesa za ununuzi.

Kwa mawasiliano zaidi juu ya uuzaji wa nyumba hizi wasiliana na Kitengo cha Mauzo **simu namba 0754 444 333; barua pepe: sales@nhctz.com** na pia tembelea tovuti ya Shirika **www.nhctz.com**.

**IMETOLEWA NA:**

**KITENGO CHA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII**

**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**

